TANGAZO LA SERIKALI NA. 85 la tarehe 17/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA 355)

---

# AMRI

---

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

---

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA BUSENGWA YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Busengwa ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale.

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 461624.461MS, 9646476.672KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa 97.3$^0$ hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 462381.124MS, 9646575.650KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa 110.44$^0$ kwa umbali wa kilomita 1.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 463237.349MS, 9645616.131KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa 160.27$^0$ kwa umbali wa kilomita 0.45 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 463509.231MS, 9645249.014KZ baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa 155.8$^0$ kwa umbali wa kilomita 0.39 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 463856.658MS, 9645076.419KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa 107.24$^0$ kwa umbali wa kilomita 0.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F yenye majira - nukta 463830.625MS,

9644746.393KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa 90$^0$ kwa umbali wa kilomita 1.45 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba G yenye majira - nukta 462386.723MS, 9644786.858KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa 132.4$^0$ kwa umbali wa kilomita 1.15 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H yenye majira - nukta 461664.146MS, 9645719.985KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa 155.35$^0$ kwa umbali wa kilomita 0.75 hadi ulipoanzia.''

Dodoma,
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*